# BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 05 Juni, 2025**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

309. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Zanzibar imejaaliwa kuwa na fukwe nzuri ambazo zimekuwa kivutio kizuri kwa watalii kutoka maeneo mbali mbali duniani. Hata hivyo, kumekuwa na utupaji wa taka na uchafuzi katika fukwe hizo, hali inayoondoa sifa nzuri za fukwe zetu.

(a) Je, kuna mikakati gani endelevu ya kuzuia utupaji wa taka katika fukwe za bahari yetu.

(b) Je, Mamlaka za usimamizi wa mazingira zimefanya tathmini ipi ya kujua athari za utupaji taka katika maeneo ya bahari kwa maisha ya viumbe wa baharini na binaadamu.

(c) Je, maeneo gani ya bahari yameathirika zaidi na utupaji wa taka.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

165. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tatizo la mlimbikano wa majaa bado ni kikwazo kikubwa kwa wananchi wa jimbo la Mwanakwerekwe.

Je, ni lini Wizara yako itafanya jitihada za makusudi za kuyaondoa majaa yaliyopo katika jimbo hilo, ikiwa ni pamoja na jaa la Zone F, Bondeni na lile la Mikarafuuni.

## Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

45. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Yapo malalamiko kutoka kwa wananchi na watumiaji wa benki zetu za ndani kwamba wanatozwa gharama kwa miamala ya ndani (internal transfer) kinyume na miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania (BOT) juu ya benki kutotoza ada (charges) kwa miamala yote ya ndani.

(a) Je, ni lini Serikali ililitambua tatizo hili la benki kuwatoza wateja wake gharama kwa miamala ya ndani.

(b) Je, ni ipi adhabu kwa benki ambazo zimefanya jambo hili kwa muda mrefu kinyume na miongozo ya BOT.

(c) Je, ni upi muongozo wa utozaji ada kwa watumiaji wa ‘Saving Accounts’ pale mteja anapofanya malipo ya fedha za kigeni.

## Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

210. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

(a) Tathmini ya uwekezaji wa wazawa katika sekta ya utalii iko vipi.

(b) Kwa kiasi gani kukua kwao ni sehemu ya mashirikiano wanayoyapata kutoka Serikalini.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

18. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Kilimo cha mpunga ni moja kati ya kilimo kinachotegemewa sana na wakulima walio wengi hapa kwetu Zanzibar, ijapokuwa yako maeneo bado hayajafikiwa na huduma muhimu ya umwagiliaji ndani ya mabonde hayo.

    (a) Je, kwa kiasi gani Serikali inalitambua suala hili.

    (b) Ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali za kukiimarisha kilimo hiki nchini.

168. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Kwa kuwa wananchi wanalima kilimo cha kisasa na mbegu wanayotumia haileti tija nzuri.

    Je, tuna mpango gani wa kuwapatia mbegu iliyo bora zaidi.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

133. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

    Kumekuwepo deni kubwa na la muda mrefu la wapangaji wa nyumba za Shirika la Nyumba Zanzibar.

    (a) Je, Serikali ina mpango gani juu ya kulipwa kwa deni hilo.

    (b) Kwa nini Wizara yako isiweke utaratibu wa kuzikodisha nyumba hizo kwa mfumo wa mikato ya aina yoyote kwa mkodishwaji anaekodishwa.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

40. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

    Kisiwa cha Pemba kina utajiri wa uzalishaji wa matunda kama maembe, mafenesi na kadhalika. Ukosefu wa kiwanda cha

kutengeneza juisi, kimepelekea utajiri huu kupotea na wananchi kubaki maskini.

(a) Serikali inautambua vipi utajiri huu unaopotea bila ya kufanyiwa kazi.

(b) Ni lini Serikali itajenga kiwanda cha kutengeneza juisi kisiwani Pemba ili kuwaongezea kipato wananchi wake.

(c) Je, Serikali imefanya juhudi gani za kutafuta wawekezaji katika eneo hili la kujenga kiwanda cha juisi kisiwani Pemba.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

204. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamatuni na Michezo:

Ni yepi matarajio ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) katika kuingia kwenye ushindani na vyombo vyengine vya habari kwa miaka ijayo.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

57. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasialiano na uchukuzi:

Serikali inaweka miundombinu mingi ya barabara bila ya kuweka mizani za kupimia uzito wa magari yanayotakiwa kupita katika barabara hizo na kupelekea magari makubwa yanayozidi kiwango kupita na kuziharibu barabara hizo.

(a) Je, kwa tathmini ni mizani ngapi Serikali imeweka na katika barabara zipi za Unguja na Pemba.

(b) Je, ni lini Serikali itaongeza mizani kwa ajili ya kupima uzito wa magari yanayopita katika barabara zetu, ili kupunguza athari kwa miundombinu hiyo.

(c) Je, ni ipi mikakati ya Serikali ya kuilinda mindombinu hii ya barabara ambayo imetumia fedha nyingi za wananchi katika ujenzi wake.

71. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Azma ya Mheshimiwa Rais wetu ni kuwarahisishia wananchi wake maisha bora kupitia usafiri na kutafuta wakandarasi wa kujenga barabara katika nchi nzima.

Je, kuna masharti gani wanayopewa wakandarasi hawa wakati wanakabidhi barabara hizi.

<u>**Wizara ya Afya:**</u>

48. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa mujibu wa Ripoti za Chama cha Madaktari wa Macho, Tanzania inakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa madaktari wa macho katika hospitali za umma.

(a) Je, kwa mujibu wa Serikali ni ipi takwimu rasmi ya upatikanaji wa madaktari wa macho kwa upande wa Zanzibar.

(b) Je, ni ipi 'ratio' ya madaktari wa macho katika hospitali za umma Zanzibar katika hospitali za Wilaya.

(c) Je, ni upi mkakati wa Serikali katika kutatua tatizo la kupatikana madaktari bingwa wa macho Zanzibar.

286. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali kupitia Wizara ya Afya imetenga rasilimali nyingi ikiwemo ununuzi wa madawa ili kuboresha afya za wananchi wake. Hivi sasa watu wengi kutoka nje ya Zanzibar wanatumia fursa hii ya kupata matibabu bure kuja kutibiwa Zanzibar, hali inayoongeza mzigo mkubwa kwa Serikali kununua madawa ili kufidia uhaba huo.

Je, ni lini Serikali itaona haja na kuweka utaratibu wa mfumo thabiti wa utambulisho wa kupata matibabu kwa wananchi wake ili waweze kunufaika ipasavyo na huduma za afya bora nchini.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

87. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

    Ni lini Wizara yako itawasaidia wakulima wa chumvi ili kuhakikisha kuwa mazao yao yanapata soko la uhakika.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

52. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Kumekuwa na mtazamo hasi wa kuwashirikisha walimu wenye ulemavu katika skuli zetu kwa kutegemea ulemavu wao. Wengi wanakumbwa na changamoto mbali mbali ikiwemo na kukosa vifaa maalumu vya kujifunzia na kufundishia katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

    (a) Je, ni kwa namna gani Serikali inawashajiisha na kuwasaidia walimu wenye ulemavu katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

    (b) Je, kwa takwimu ni walimu wangapi wenye ulemavu wameajiriwa katika skuli za Serikali na binafsi.

    (c) Je, Sera ya Elimu Zanzibar inazungumzia vipi suala la kuwashajiisha watu wenye ulemavu katika skuli za Serikali na binafsi.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

158. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

    (a) Nini dhamira na malengo ya kujengwa mabafu ya kiajemi yaliyopo katika mtaa wa Hamamni mjini Zanzibar.

    (b) Kwa kiasi gani mabafu haya yana upekee katika kuilezea historia na utamaduni wa Mzanzibari.

II. **<u>HOJA ZA SERIKALI:</u>**

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2025/2026.

Zanzibar,
05 Juni, 2025.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR